SEBHA UNIVERSITY JOURNAL OF HUMAN SCIENCES VOL.25 NO. 1 2026
DOI: 10.51984/w3QYP205

جامعة سبها للعلوم الإنسانية مجلة
Sebha University Journal of Human Sciences

Journal homepage: http://www.sebhau.edu.ly/journal/johs

# Chimbuku la Ushairi wa Kiswahili

Bubaker Owhida Ahmed Owhida

Department of African Languages and Studies, Faculty of Languages, Sebha, libya

**Maneno muhimu :**
Mamboleo
Mapokeo
Mizani
Urari
Ushairi
Vina
Wanasasa
Chimbuku la Ushairi wa Kiswahili.

**MUHTASARI:**
Ushairi ni utanzu muhimu wa fasihi katika jamii nyingi husus ani za Kiafrika katika kupitisha maudhui mbalimbali ya jamii. Ushairi wa Kiswahili ndio utanzu mkongwe zaidi wa fasihi. Ushairi huu umepitia mabadiliko mengi, mabadiliko haya yapo katika upande wa maudhui, miundo na mitindo ya lugha inayotumiwa, Mashairi hayo yamepitia hatua za usimulizi, maandishi ikiwa awali ni kwa hati ya Kiarabu na baadaye hati ya Kirumi/ Kilatini. Makala hii katika sehemu yake ya kwanza inajadili dhana ya ushairi ya Kiswahili kwa mitazamo ya wataalamu mbalimbali wa mikabala miwili tofauti yaani mkabala wa kimapokeo au wanamapokeo na mkabala wa kimamboleo au wanasasa Sehemu ya pili ya makala hii inatalii chimbuko la ushairi wa Kiswahili na inajadili hoja mbili, kuhusu mada hii na ubora na udhaifu wa kila hoja. Hoja ya kwanza inadai kuwa; chimbuko la ushairi wa Kiswahili ulitokana na ujio wa Waarabu. Na hoja ya pili inasema kuwa; chimbuko la ushairi wa Kiswahili ni zao la jamii ya waswahili wenyewe.

# مصادر الشعر السواحيلي

ابوبكر اوحيدة احمد اوحيدة

قسم اللغات والدراسات الأفريقية ، كلية اللغات، جامعة سبها، ليبيا

**الكلمات المفتاحية:**
الحداثة
التراث
الوزن الشعري
الاتزان الإيقاعي
الشعر
القافية
المعاصرون

**الملخص**
الشعر واحداً من أشكال الفن الأدبي في اللغة، وهوا نوع أدبي مهم في العديد من المجتمعات وخاصة في أفريقيا، ويعد الشعر السواحيلي أقدم نوع من أنواع الأدب السواحيلي، ولقد خضع هدا الشعر للعديد من التغيرات في سياق المحتوى والبنية والأنماط الخاصة باللغة السواحيلية، وكانت البداية كتابة النص الشعري باللغة السواحيلية في الأصل بالخط العربي، ولاحقاً بالخط الروماني / اللاتيني
تناقش هده المقالة في جزئها الأول مفهوم الشعر السواحيلي من اتجاهين مختلفين هما النهج التقليدي والنهج الحديث.
ويستكشف الجزء الثاني من هده المقالة أصول الشعر السواحيلي ويناقش نظريتين، حول هدا الموضوع ويبحث في نقاط القوة والضعف في كل نظرية، تدعي النظرية الأولى أن أصل الشعر السواحيلي يرجع إلى قدوم العرب الي شرق افريقيا، فيما تدعي النظرية الثانية أن أصول الشعر السواحيلي هي نتاج المجتمع السواحيلي نفسه.

**Utangulizi**:
Makala hii lilikuwa ni kuchunguza **Dhana** na **Chimbuku la Ushairi wa Kiswahili** Katika **sehemu ya kwanza** tutajadili dhana ya ushairi ya Kiswahili kwa mitazamo ya wataalamu mbalimbali wa mikabala miwili tofauti yaani mkabala wa **wanamapokeo** ambao wanasisitiza vina na urari wa mizani, kama Mnyampala, Abdalla … n.k. na mkabala wa **wanausasa** wao wanaonekana kupuuza masharti ya vina na urari wa mizani katika ushairi, kama Mulokozi, Kahigi… n.k.

**Sehemu ya pili** ya makala hii tutajadili chanzo, asili au chanzo cha ushairi wa Kiswahili kutokana na mitazamo ya wataalamu mbalimbali wa Kiswahili na maelezo tofauti waliyotoa kuhusu chanzo cha ushairi wa Kiswahili na tutajaribu kujibu swali yafuatayo:

Je; Ushairi wa Kiswahili ulianza lini?

Chimbuko la ushairi wa Kiswahili ulitokana na ujio wa Waarabu au ni ni zao la waswahili wenyewe?

**1. Dhana ya Ushairi:**

Dhana ya ushairi imefasiliwa na wataalamu mbalimbali. Miongoni mwa wataalamu hawa ni Amri Abeid (1954:1) anayesema kuwa "ushairi au utenzi ni wimbo, hivyo kama shairi haliimbiki halina maana."

Ushairi umefasiliwa na Mnyampala (1970) kuwa ni msingi wa maneno ya hekima tangu kale ndicho kitu kilichobora sana maongozo ya dunia kwa kutumia maneno ya mkato na lugha nzito yenye kunata iliyopangwa kwa urari wa mizani na vina maalum.

Abdalla (1974) anaeleza kuwa ushairi ni utungo ambao katika kila ubeti wake kuna ulinganifu wa vina vitukufu vilivyopangwa kimoja baada ya chenziye; wenye vipande vilivyo na ulinganifu wa mizani

*Corresponding author:
E-mail addresses: Abu.almajry@sebhau.edu.ly
*Article History : Received 02 August 2025 - Received in revised form 30 December 2025 - Accepted 16 January 2026*

zisizo pungufu wala zilizo zaidi.

Mulokozi na Kahigi (1982:25) wanasema ushairi ni "sanaa inayopambanuliwa kwa mpangilio maalum na fasaha na wenye muwala, kwa lugha ya picha, sitiari au ishara katika usemi, maandishi au mahadhi ya wimbo ili kuleta wazo au mawazo, kufunza au kueleza tukio au hisia fulani kuhusu maisha au mazingira ya binadamu kwa njia inayogusa moyo."

Aidha, Njogu na Chimerah (1999) wanafasili ushairi kuwa ni sanaa ya lugha inayoeleza jambo au wazo kwa njia ya mkato na kwa namna inavyoteka hisia za msomaji au msikilizaji. Waendelea kuelezea kuwa maneno ya mashairi huteuliwa kimaksudi ili yalete taswira maalumu akilini kwa msomaji au msikilizaji. Maneno hayo hupangwa ili yatoe mdundo fulani wa shairi linapoimbwa, linaposomwa, linapoghaniwa au linaposemwa.

Mssamba, (2003) akimnukuu Shaban Robert, anasema; "ushairi ni sanaa ya vina inayopambanuliwa kama nyimbo, mashairi na tenzi zaidi ya kuwa na sanaa ya vina ushairi unaufasaha wa maneno machache au muhtasari."

Encyclopedia American (EA) inaeleza kuwa ushairi ni kauli zenye hisia na ubunifu, mpangilio fulani wenye urari, uwasilishaji wa tajiriba au mawazo ya mtunzi kwa maana ambayo huibua tajiriba kama hiyo katika nyayo za wasomaji au wasikilizaji na kutumia lugha ya picha yenye wizani wa sauti.

Owheda (2006) katika utafiti wake anasema kwamba wafuasi wa mkondo wa ushairi wa kimapokeo wanaonekana kusisitiza vina na kuwa urari wa mizani ni uti wa mgongo wa ushairi. Hivyo, iwapo utungo hautakuwa na urari wa vina na mizani na hautaimbika, utungo huo hauwezi kuwa ushairi.

Na anasisitiza kuwa ama kwa wanausasa wao wanaonekana kupuuza masharti ya vina na urari wa mizani katika ushairi. Wafuasi wa mkondo huu wanasisitiza kuwa ili utungo uwe ushairi lazima kuwepo na uwiano wa fani na maudhui.

Hivyo basi kutokana na dhana hii ya ushairi hufasiliwa na wataalamu mbalimbali wa mikabala miwili tofauti yaani mkabala wa kimapokeo au wanamapokeo (Mavina) na mkabala wa kimamboleo au wanasasa (Masivina) tunaweza kusema kuwa ushairi ni kazi ya sanaa yenye kuandikwa au kuimbwa kwa kufuata kanuni za ushairi au kutofuata kanuni za ushairi ikiwa na maana kuwa ushairi waweza kuwa wa kimapokeo au wa kisasa ilimradi ushairi huo uwe na ujumbe.

**2. Chimbuko la Ushairi wa Kiswahili:**

Dhana ya chimbuko inafasiriwa na TUKI (2004) kuwa ni mwanzo au asili ya kitu. Katika andiko hili, dhana ya Chimbuko, inamaanisha asili au chanzo cha jambo fulani. Hivyo, kusema chimbuko la ushairi wa Kiswahili tunamaanisha asili au chanzo cha ushairi wa Kiswahili.

Katika (Owheda 2006)" Sheikh Alamin bin Ali Almazrui (1891-1947) akitumia mkono aliandika kitabu cha kwanza cha ushairi wa Kiswahili kwa hati ya Kiarabu. Kitabu hicho kilihusu elimu ya Arudhi ya Kiswahili aliyokiita Arudhi." Kitabu hiki, kinapatikana SOAS-London.

Wataalamu mbalimbali walijadili chimbuku la ushairi wa Kiswahili na wametoa maelezo tofauti kwa kuzingatia mitazamo au nadharia mbili ambazo ni kama ifuatavyo: Nadharia ya kwanza inadai kuwa;

Chimbuko la ushairi wa Kiswahili ulitokana na ujio wa Waarabu. Na nadharia ya pili inasema kuwa; Chimbuko la ushairi wa Kiswahili ni zao la jamii ya waswahili wenyewe.

**2.1 Nadharia ya Kwanza:**

Kwa kuanza na nadharia ya kwanza isemayo kuwa chimbuko la ushairi wa Kiswahili ulitokana na ujio wa Waarabu ambayo inaungwa mkono na wataalam mbalimbali kama vile Lyndon Harries (1962) na Knappet (1979).

Kwa kuanza na Lyndon (1962) "Swahili Poetry" anatoa hoja tatu ambazo ni ushairi wa Kiswahili umetokana na Uislamu, ushairi ulianzia kwenye upwa wa kaskazini mwa Kenya hususani Lamu. Na maudhui ya ushairi wa Kiswahili yalitokana na ushairi wa Kiarabu. Utungo wa kwanza wa ushairi andishi wa Kiswahili ni Tambuka, Mwengo bin Athmani (1728).

Ubora wa nadharia hii au mtazamo wa Harries kuhusu chimbuko la ushairi wa Kiswahili ni kwamba umesaidia wengine kuendelea kuchunguza zaidi kuhusu chimbuko la ushairi wa Kiswahili.

Udhaifu wa nadharia hii ni kuwa si kweli kwamba ushairi wa Kiswahili uliletwa na Uislamu bali ulikuwepo hata kabla ya ujio wa Uislamu, kwani ushairi hautenganishwi na jamii husika. Hivyo jamii za waswahili walitumia nyanja mbalimbali za ushairi katika shughuli zao mbalimbali au shughuli zao za kila siku, kama vile; shughuli za kilimo na ufugaji.

Pia ushairi wa Kiswahili ulianza karne ya 10BK na ushairi wa Kiswahili ulikuwa ukitungwa na kughanwa kwa ghibu bila kuandikwa. Wataalam wengi wanakubaliana kuwa asili ya ushairi wa Kiswahili ni tungo simulizi hasa ngoma na nyimbo.

Udhaifu mwingine katika mtazamo wake wa kusema kuwa ushairi ulianzia pwani ya kaskazini ya Kenya si kweli kwa kuwa waswahili walikuwepo hata sehemu nyingine kama vile Kilwa na Bagamoyo ambapo ushairi wa Kiswahili ulitumika.

Ubora wa hoja hii ni kwamba, ni kweli Knappert amekubali kuwa,ushairi wa Kiswahili ulitokana na waswahili wenyewe. Hata hivyo hoja yake ina udhaifu kwa kuwa ushairi wa Kiswahili ulianza kabla ya karne ya 10 BK na pia amejikita katika maudhui ya mambo mengine kama vile siasa, uchumi na kijamii. Vilevile amechanganya chimbuko la ushairi wa Kiswahili na Uarabu.

**2.2 Nadharia ya pili:**

Nadharia ya pili inasema kuwa ushairi ni zao la waswahili wenyewe. Nadharia hii imejadiliwa na wataalam mbalimbali akiwemo Shaban Robert, Jumanne Mayoka (1993) na Senkoro, Mulokozi na Sengo.

Jumanne, M. Mayoka (1993) anasema ushairi umetokana na jamii ya wanadamu wenyewe na umesheheneza ukwasi mkubwa wa lugha ambayo imekuwa ikitumika katika hatua zote za kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni katika historia ambayo mwanadamu amepitia, Kwa mfano kuwa msamiati uliotumika tangu enzi za kuishi mapangoni, enzi za uwindaji, ujima, utumwa, vita vya makabila, uvamizi wa wageni, ukoloni na harakati za kupambana na ukoloni hadi kupata uhuru na maendeleo yake.

Ushairi wa Kiswahili na wa makabila mengine ya Afrika nzima ni wa zamani sana na wala hauna tarehe. "Waarabu waliukuta ushairi wa Kiswahili, wakautumia" Oheda (2006).

Na anaendelea kusema kuwa "Waswahili hawakuzichukuwa tungo za ushairi wa Kiarabu hivyo hivyo na kuzitia katika ushairi wa Kiswahili (shilingi kwa ya pili) bali waswahili wamezifanyia marekebisho".

Ubora wa hoja hii ni kwamba ina mashiko ndani yake kwa sababu, kila jamii ina sanaa yake na ushairi ni moja kati ya sanaa hizo ingawa inaweza ikaathiriwa na sanaa ya jamii nyingine. Pia ushairi umekuwa ukikua na kuendelea kadri jamii inavyokuwa na kuendelea.

Udhaifu wa hoja hii ni kwamba si kweli kuwa katika kipindi hicho ushairi ulikuwa tayari umesheheni ukwasi mkubwa wa lugha, na kama ulikuwa kweli umesheheni huu ukwasi wa lugha alipaswa kutuonesha huo utajiri wa lugha anaouzungumzia katika ushairi.

Senkoro (1988) anasema kuwa ushairi uliibuka pale lugha ilipoanza katika kipindi cha uhayawani (kipindi ambacho mwanadamu alipoanza kupambana na mazingira yake) kwenda katika kipindi cha urazini (maana) ili kumwezesha binadamu na mazingira yake kwa mfano, zana za kazi zilizotumika ziliwafanya waimbe kwa kufuata mdundo wa zana hizo.

Ubora wa hoja hii ni kwamba unathibitisha kuwa chimbuko la ushairi ni waswahili wenyewe, kwani umefanikiwa kueleza kuwa katika jamii yoyote ile maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii huambatana au huenda sambamba na maendeleo ya sanaa mbalimbali ikiwemo ushairi uliotumika katika harakati mbalimbali za maisha ya mwanadamu.

**Hitimisho:**

Baada ya kuangalia fasili mbalimbali za nadharia ya Ushairi wa Kiswahili kwa wataalamu wa mikabala miwili (kimapokeo) na (kimamboleo) tunaweza kusema kuwa ushairi ni kazi ya sanaa yenye kuandikwa au kuimbwa kwa kufuata kanuni za ushairi au kutofuata kanuni za ushairi, ama kwa kuhusu Chimbuko la ushairi wa Kiswahili tulipitia nadharia mbili; nadharia ya kwanza inadai kuwa; Chimbuko la ushairi wa Kiswahili ulitokana na ujio wa Waarabu, na nadharia ya pili inasema kuwa; Chimbuko la ushairi wa Kiswahili ni zao la jamii ya waswahili wenyewe na tulipata kusema kuwa ushairi ni zao la waswahili wenyewe na ushairi wa Kiswahili katika upwa wa Afrika Mashariki ulianza kabla ya ujio ya Waarabu na Waisilamu wa uswahilini waliziandika tungo zao kwa hati ya Kiarabu.

**MAREJEO:**

Knappert, J. (1979). Four centuries of Swahili Verse. Heinemann. London.

Mayoka, J.K. (1993). Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka. Ndanda Mission Press.Tanzania.

Mulokozi, M.M. (1996). Fasihi ya Kiswahili.Chuo Kikuu cha Dar-

esSalaam. Dar-es-Salaam.
Owhida, B.O.A (2006) Ushairi wa Kiswahili na Ushairi wa Kilibya, kufanana na kutofaotiana, Open University of Tanzania. Tasnifu ya Uzamivu (PhD). (Haijachapishwa).
Senkoro, F.E.M.K. (1987). Ushairi, Nadharia na Tahakiki. DUP. Dar-esSalaam.
TUKI. (1983). Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili. (Toleo la III) TUKI.Dar-es-Salaam
TUKI. (2004). Kamusi ya Kiswahili Sanifu.TUKI.Dar-es-Salaam.